

## Maswali

1. Nani alikuwa mfalme wa Wasraeli?
2. Samweli alikuwa nabii mzuri. Wanawe walikuwa wa namna gani?
3. Mbona Waisraeli walitaka mwanadamu awe mfalme wao?  
(Sababu 3)
4. Mungu alisema nini Samweli alipomuomba?
5. Mungu aliyeana ilani gani kwa watu walipotaka mfalme mwanadamu?
6. Mwana wa Kishi aliitwa nani? Alikaa namna gani?
7. Sauli na mtumishi wake walienda kutafuta nini?
8. Mambo mawili gani yenye Samweli aliaambia Sauli?
9. Samweli aliambia nini Waisraeli wote?
10. Waisraeli walipiga kelele eti nini?

## Majibu

### Note: Answer 8 missing

1. Mungu alikuwa mfalme wao.
2. Wana wa Samweli walikuwa waovu.
3. Wana wa Samweli walikuwa waovu kwa hivyo hawangekuwa vingozi wazuri. Walitaka mfalme mwanadamu mwenye wangeona kama mataifa mengine. Walitaka mfalme atakaye wapeleka vitani.
4. Wamenikataa Mimi sio wewe, Samweli. Waache wawe na mfalme.
5. Watakuwa wakilipa kodi kwa mfalme. Atachukua wana wao kuwa askari, binti wao kuwa watumishi tena atachukua kondoo na mbuzi wao.
6. Mwana wa Kishi aliitwa Sauli. Alikuwa mrefu, sura nzuri na wa nguvu.
7. Sauli na mtumishi wake walienda kutafuta punda wa Kishi.
9. Mungu amemchagua huyu kuwa mfalme wenu. Nimrefu kuliko nyinyi nyote.
10. Waisraeli walitoa sauti na kusema, "Mungu saidia Mfalme."

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

**Awamu ya 1   Mwaka wa 3**



## 24 Saulo ni Mfalme

### Marejeo

1 Samweli 8:4 – 6; 9:1 – 3 na 15 – 17; 10:1 na 24

### Kiini cha somo

Kuonyesha vile Waisraeli walitaka kuwa kama mataifa mengine lakini Samweli alibaki mwaminifi kwa Mungu.

### Maneno maalum

- 24.1 Waisraeli + Mungu alikuwa Mfalme wao + wanataka mfalme mwanadamu + Samweli + watoto waovu + wakuu + wanataka mfalme mwanadamu
- 24.2 Samweli + aliomba + Mungu + wape mfalme + ilani + wanataka mfalme mwanadamu + kwa vita + mrefu tena wa nguvu
- 24.3 Kishi + punda wamepotea + tuma Sauli + hakupata punda
- 24.4 Mtumishi + Samweli + punda wamepatikana + Sauli awe mfalme
- 24.5 Samweli + Waisraeli wote + Sauli + mrefu zaidi + mfalme wenu + Mungu saidia mfalme

**24.1** Waisraeli hawakuwahi kuwa na mfalme mwanadamu kuwatawala kwa sababu Mungu alikuwa Mfalme wao. Mataifa mengine karibu na Waisraeli walikuwa na wafalme waliowatawala, lakini Mungu alikuwa Mfalme wa Waisraeli. Mungu alipea Waisraeli nchi yao na sheria na maagizo ya kuwasaidia kuishi. Alikuwa Mungu wao na Mfalme wao. Walikuwa watu wakipekee wa Mungu.

Mtoto Samweli alikuwa na akawa nabii mzuri. Alimtumkia Mungu na kuwasaidia Waisraeli kwa miaka mingi. Aliwafundisha kumpenda Mungu na kumtii.

Samweli alipokuwa mzee, hakuweza kufanya kazi nyingi. Aliwaambia wanawe wawili wamsaidie. Watu walipenda kuenda kwa Samweli awasaidie kwa sababu alikuwa mzuri tena haki. Lakini hao wana wa Samweli wawili walikuwa waovu. Wakati mwininge walichukua hongo na kuwa na uamzi mbaya.

Siku moja wazee wa Israeli walikuja kwa Samweli na kumwambia, "Wewe ni mzee na wanao hawatendi kama wewe. Tunataka utuchagulie mfalme mwanadamu kama mataifa mengine." Hii ilimkasirisha Samweli sana. Samweli alipenda Mungu. Alijua vile Mungu alikuwa na hekima na vile alikuwa na upendo kwa watu wake. Tena alikumbuka vile Mungu alikuwa amewapigania vita kwa maadui wao.

**24.2** Samweli alikuwa na huzuni sana. Aliomba Mungu na kumuuliza afanye nini. Mungu aliambia Samweli, "Watu wamekataa mimi kuwatawala. Hawajakukataa wewe. Wasikilize na uwape mfalme. Lakini uwahadharishe vile itakuwa na huyo mfalme."

Samweli alizungumza nao na kuwambia ilani za Mungu. Mfalme atawashurutisha kulipa kodi. Atawachukuwa wanaume wenu kwenda kupigana kwa jeshi lake. Atachukuwa wana wenu na binti wenu kuwa watumishi wake. Atachukuwa kondoo na mbuzi wenu ale pamoja na watumishi wake.

Lakini watu hawakusikia ilani ya Mungu. Waliambia Samweli, "Tunataka mwanadamu awe mfalme na atutawale. Ili tuwe kama mataifa mengine yote. Tunataka mfalme atuongoze kwa vita ili tupigane na maadui wetu.

Waisraeli walitaka mfalme wakuwaongoza kwa vita. Walitaka mtu mnene, mrefu, aliye na zura nzuri na wa nguvu. Mungu aliwawezesha kuwa na mfalme wa aina waliyetaka.

**24.3** Kulikuwa na mtu aliyeitwa Kishi. Alikuwa tajiri sana na watumishi wengi na punda wengi. Siku moja punda wake wakapotea. Watumishi wake hawakuwaona po pote. Kishi alikuwa na mwana aliyeitwa Sauli. Sauli alikuwa mrefu na sura nzuri, tena mrefu kuliko watu wote. Kishi aliambia Sauli achukue mtumishi mmoja na waende kutafuta punda.

Sauli na mtumishi walienda kutafuta punda. Walitembea kwa muda mrefu lakini hawakupata punda. Punda walikuwa wa maana sana kwa Kishi. Sauli alitafuta sana kwa bidii. Lakini mwishowe aliambia mtumishi, "Hatuwezi kupata punda po pote. Itatubidi turudi nyambani."



**24.4** Mtumishi aliambia Samweli kwamba anajua nabii wa Mungu aliyeishi karibu na walikokuwa. Labda anawenza kutwambia penye punda wako. Walipofika mjini walikutana na nabii Samweli. Mungu alikuwa ameambia Samweli kwamba Sauli atakuja mjini siku hiyo. Mungu alimwambia kwamba alikuwa amechaguwa Sauli kuwa mfalme wa Israeli. Samweli alikutana na Sauli na mtumishi wake. Aliambia Sauli kwamba punda walikuwa wamepatikana. Tena alimwambia kwamba yeze atakuwa mfalme wa Israeli. Sauli alishangaa sana!

**24.5** Samweli aliita watu wote wa Israeli kukuja pamoja na waone mfalme wao. Sauli aliposimama mbele yao alikuwa mrefu kuliko watu wote. Samweli aliambia watu, "Huyu ndiye mtu Mungu amemchagulia kuwa mfalme wenu. Yeze ni mrefu kuliko nyinyi wote."

Halafu watu wote walipiga kelele, "Mungu saidia Mfalme."